TALKING NOTES ZA MHE. THOBIAS E. M. ANDENGENYE, MKUU WA MKOA WA KIGOMA WAKATI AKIZUNGUMZA NA WAJUMBE WA BARAZA LA MADIWANI LA HALMASHAURI YA WILAYA KIBONDO
TAREHE 14 JUNI, 2021

UTANGULIZI

Mhe. Habili Charles Maseke - Mwenyekiti wa Halmashauri,

Mhe. Louis Peter Bura - Mkuu wa Wilaya,

Mhe. Norbert Godwin Bulinjiye - Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri,

Ndg. Diocles Mugishagwe Rutema - Mkurugenzi Mtendaji (W),

Ndg. Valence Rutakyamirwa - Mkaguzi Mkuu wa Nje (NAOT),

Ndg. Hamis Tahiro - Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya,

Ndg. Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Ndg. Wajumbe wa Kamati ya Usalama ya Wilaya,

Wah. Madiwani,

Ndg. Watendaji katika ngazi mbalimbali,

Ndg. Wageni Waalikwa,

Ndg. Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri,

- Natoa Shukrani kwa Uongozi wa Wilaya ya Kibondo na Halmashauri ya Wilaya Kibondo kwa Mwaliko wa kushiriki na kuzungumza na Wajumbe wa Baraza la Madiwani na Wananchi waliofika kufuatilia Mkutano huu Maalum wa kujadili **Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020**.

- Hii ni mara yangu ya kwanza kupata nafasi ya kuzungumza nanyi katika Baraza lenu tangu nilipoteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma.

- Hili ni jambo la heshima kwangu kwani nitapata fursa ya kusikiliza namna mnavyoendesha majadiliano yenu na kuwashauri kadri itakavyohitajika wakati Mkutano ukiendelea.

- Nawapongeza kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yenu licha ya changamoto kadhaa mnazokabiliana nazo.

- Nawashukuru nyote kwa mahudhurio yenu mazuri.

TAARIFA YA CAG KWA HESABU ZA MWAKA 2019/2020

Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri,

- Nimesoma Ripoti Kuu ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo pamoja na mambo

mengine imeonesha kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekagua na kutoa hati kwa Mamlaka 185 za Serikali za Mitaa. Kati ya Mamlaka hizo 185; Halmashauri 124 sawa na asilimia 67 zilipata hati inayoridhisha, Halmashauri 53 sawa na asilimia 29 zilipata hati zenye shaka na Halmashauri 8 sawa na asilimia 4 zilipata hati mbaya.

- Kama mnavyofahamu, Halmashauri yenu ni miongoni mwa Halmashauri mbili katika Mkoa wetu zilizopata Hati Inayoridhisha. Halmashauri nyingine ni Halmashauri ya Wilaya Kigoma.

- Nawapongeza kwa kupata Hati inayoridhisha (Hati Safi) kwa mwaka wa nne mfululizo (MF 2016/2017, MF 2017/2018, MF 2018/2019 na MF 2019/2020). *Endelezeni ushirikiano mlioujenga baina yenu na zingatieni Sheria na Taratibu ili kuweza kupata Hati za Ukaguzi zinazoridhisha kila mnapokaguliwa.*

- Halmashauri 6 katika Mkoa wetu zilipata Hati yenye Shaka na hivyo kututia doa kama Mkoa. Halmashauri hizo ni; Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji, Halmashauri ya Mji Kasulu, Halmashauri ya Wilaya Buhigwe, Halmashauri ya Wilaya Kakonko, Halmashauri ya Wilaya Kasulu na Halmashauri ya Wilaya Uvinza.

- Pamoja na kupata Hati inayoridhisha, Halmashauri yenu pia ni miongoni mwa Halmashauri 93 nchini (na 4 katika Mkoa wa Kigoma) zilizopata Aya ya Masuala ya Mkazo *(Emphasis of Matters)*.

- Halmashauri yenu pia ni miongoni mwa Halmashauri zilizofanyiwa Ukaguzi Maalum katika kipindi cha mwaka 2019/2020 (Ukaguzi huo ni kwa miaka mitatu 2017/2018, 2018/2019 na 2019/2020). Baadhi ya mapungufu yaliyobainika yamejumuishwa katika Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2019/2020. Baadhi ya mapungufu hayo ni;

  - Ukaguzi Maalumu ulibaini kuwa Halmashauri ilishindwa kukusanya mapato ya ushuru wa huduma kiasi cha sh. 111,026,052, kutokana na shughuli mabalimbali za kiuchumi zilizofanyika ndani ya Halmashauri.

    Upotevu huu wa mapato unatokana na udhaifu wa Halmashauri kushindwa kufuatilia vyanzo vya mapato ikiwemo ushuru wa huduma ili kujua kampuni na wadau wote wanaoendesha shughuli za kiuchumi ndani ya maeneo yenu ya kiutawala na kuhakikisha kuwa yanalipa ushuru kadri ya matakwa ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Na. 9 ya 1982 (kama ilivyorekebishwa 2000).

    Nawashauri mwongeze nguvu katika kufuatilia na kujua mapato halisi ya Taasisi zinazofanya kazi au kutoa huduma ndani ya maeneo yenu ya kiutawala kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ili muweze kukusanya mapato stahiki kutoka katika taasisi hizo.

- Ukaguzi Maalum ulibaini kuwa Fedha za mradi wa maji Mgoboka (sh. 22,000,000) zimetumika kulipa gharama za umeme zilizotakiwa kulipwa na Mamlaka ya Maji Kibondo Mjini. *Ninaelekeza hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya Watendaji wa Halmashauri kama walivyotajwa kwenye ripoti ya Ukaguzi Maalumu kwa kushindwa kusimamia fedha za Serikali na kupelekea matumizi mabaya ya fedha. Aidha, Halmashauri ihakikishe inarejesha fedha hizo kwenye mradi husika.*

- Hati za Malipo ya sh. 162,556,940 hazikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi wakati wa Ukaguzi Maalum. *Naelekeza hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watendaji walioshindwa kuwasilisha nyaraka hizo kwa kutokuwa makini katika utunzaji wa hati za malipo. Aidha, Menejimenti inashauriwa kuimarisha taratibu za kuhifadhi nyaraka ikiwa ni pamoja na kutenga chumba maalum kwa ajili ya kutunzia nyaraka husika.*

- Ukaguzi Maalum ulibaini kuwa Maduhuli ya jumla ya sh. 430,336,652 yalikusanywa bila kupelekwa benki. *Nawashauri muwafuatilie waliokusanya fedha hizo ili zipatikane na ziweze kupelekwa benki. Aidha, naelekeza hatua kali za kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa wahusika wote.*

- Ukaguzi Maalum ulibaini kuwa Miamala yenye thamani ya sh. 632,512,448 ilirekebishwa kwenye Mfumo wa Mapato bila Idhini

ya Afisa Masuuli na vielelezo stahiki. Hii ni kutokana na kuwepo kwa mfumo dhaifu wa udhibiti wa mapato ya ndani. *Nawashauri muimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani. Katika hali ya kawaida ya utendaji makini Mkaguzi wa Ndani anapaswa kubaini mapungufu ya aina hiyo mapema ili hatua zichukuliwe kwa wakati.*

- Pamoja na hoja hizo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebainisha mapungufu kadhaa kwenye hesabu zenu kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Baadhi ya mapungufu hayo ni;

  - Halmashauri haikuweka madeni yenye thamani ya sh. 28,320,500 kwenye taarifa ya fedha za mwaka uliopita, hivyo kusababisha kuongezeka kwa malipo nje ya bajeti. Menejimenti haikuweza kuthibitisha iwapo malipo ya madeni hayo yalitengewa bajeti kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020. Ulipaji wa madeni yasiyotambuliwa awali unasababisha kuzidishwa kwa matumizi kwa mwaka husika. *Menejimenti inatakiwa kuzingatia madeni yote yaliyopo kwenye taarifa za fedha wakati wa kuandaa bajeti.*

  - Halmashauri ilishindwa kuhamisha kwa wakati fedha za zuio (sh. 117,190,899) kwenda RUWASA. Hali hiyo inaweza kusababisha wakandarasi kutolipwa fedha zao punde miradi itakapokamilika. Natambua jitihada zilizofanyika kurejesha sehemu ya fedha hizo.

Ninaelekeza mhakikishe mnahamisha fedha zote za zuio zilizosalia (sh. 65,279,819) kwenda RUWASA ili kuepuka kuwaletea usumbufu wakandarasi.

- Kutohuishwa kwa Sheria Ndogo za kukusanya Mapato zilizotungwa mwaka 2017. Kutohuisha Sheria ndogo kunapunguza wigo wa vyanzo vya ukusanyaji wa mapato ya ndani na hivyo Halmashauri kushindwa kutoa huduma tarajiwa kwenye jamii kutokana na uhaba wa fedha. *Ninashauri mchukue hatua stahiki kuhakikisha kuwa sheria ndogo zinahuishwa ili kuimarisha hali ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, na hivyo kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali kuu.*

- Halmashauri ilitoa mikopo yenye thamani ya sh. 336,251,865 kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 kiasi cha sh. 253,956,965 kilikuwa bado hakijarejeshwa. Nimeelezwa kuwa jitihada zimefanyika na kuwezesha sh. 52,292,900 kurejeshwa na hivyo kubaki sh. 201,664,065. *Naelekeza Menejimenti ifanye ufuatiliaji wa marejesho hayo ili fedha hizo zitumike kukopesha wahitaji wengine.*

- Madai ya muda mrefu na malipo yaliyofanywa na Halmashauri kabla ya kupokea huduma (sh. 201,654,999). *Nashauri*

muongeze nguvu katika kukusanya ili shughuli zilizopangwa ziweze kutekelezwa.

- Madeni yasiyolipwa kwa muda mrefu - sh. 317,955,289. *Nawashauri muongeze kasi ya makusanyo na mjiwekee utaratibu wa kulipa madeni awamu kwa awamu na kwa yale yanayosubiri utaratibu wa HAZINA ni vyema kujiwekea utaratibu wa kuyakumbushia.*

- Halmashauri ina mashauri ambayo hayajafungwa kutokana na madai dhidi yake yenye thamani ya sh. 647,291,569 ambayo yanaweza kuathiri mtiririko endelevu wa kifedha. *Nashauri Halmashauri ishughulikie mashauri hayo kwa makini na kadri inavyowezekana imalize mashauri hayo nje ya Mahakama.*

- Halmashauri ilinunua bidhaa na huduma zenye thamani ya sh. 190,337,891 kutoka kwa Wasambazaji wasioidhinishwa na Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA). *Nawashauri mzingatie Sheria, Kanuni na Taratibu za Manunuzi ya Umma.*

- Malipo kufanywa kwa wadai kwa fedha taslimu (bila kupitia kwenye akaunti zao) sh. 39,998,070. *Nasisitiza Menejimenti kuzingatia Mwongozo wa fedha wa Serikali za Mitaa (LAAM, 2019) unaozitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya malipo*

kwa kupitia mfumo wa Kielektroniki kwa kulipa moja kwa moja kwenye akaunti za wateja.

- Halmashauri imekusanya Maduhuli jumla ya sh. 66,706,739 lakini hayakupelekwa benki. *Naelekeza Halmashauri ihakikishe maduhuli yote yanapelekwa benki na suala hili lisijirudie tena.*

- Taarifa kamili ya hoja zote za mwaka 2019/2020 na hoja za miaka ya nyuma (ambazo hazijafungwa) itawasilishwa na kujadiliwa katika Mkutano huu.

- Hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma (hadi wakati taarifa ya ukaguzi kwa mwaka 2019/2020 inatolewa) inaonesha kwamba mapendekezo 49 yalitolewa kwa Halmashauri yenu ambapo mapendekezo 17 yametekelezwa, mapendekezo 11 yako katika hatua ya utekelezaji, mapendekezo 12 yamejirudia, mapendekezo 8 hayajatekelezwa na pendekezo 1 limepitwa na wakati.

- Kwa upande wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) hali halisi ya utekelezaji kwa miaka ya nyuma inaonesha kwamba maagizo 9 yalitolewa kwa Halmashauri yenu ambapo hadi sasa maagizo 6 yako katika hatua ya utekelezaji, agizo 1 limejirudia na maagizo 2 hayajatekelezwa.

- Nashauri mjiwekee mkakati madhubuti wa kutekeleza mapendekezo yote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya miaka ya nyuma yaliyosalia pamoja na kutekeleza maagizo yote ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ya miaka ya nyuma yaliyosalia.

MAELEKEZO YA NYONGEZA KUHUSU TAARIFA YA CAG

Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri,

- Katika mkutano wa leo mnalo jukumu la kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria Watumishi waliobainika kuhusika na vitendo vya ubadhirifu (kama wapo) na kutowajibika ipasavyo na hivyo kuiletea Halmashauri yenu hasara na hoja ambazo katika hali ya kawaida ya utendaji makini zisingepaswa kutokea. Uchukuaji huu wa hatua ulenge Watumishi wote waliohusika katika ngazi zote (ngazi za chini, kati na Makao Makuu ya Halmashauri).

- Hakikisheni mnaimarisha uwajibikaji kwenye usimamizi wa fedha na rasilimali nyingine, zingatieni taratibu za fedha na imarisheni mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuepuka kupata Hati Isiyoridhisha.

- Nidhamu na Uadilifu kwa Watendaji ni muhimu. Watumishi wenye tabia zisizokubalika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma wajirekebishe na wasiposikia wachukuliwe hatua. **Msilee utovu wa Nidhamu**.

- Hakikisheni hoja za ukaguzi zinajibiwa mapema na majibu kuwasilishwa kwa Mkaguzi Mkuu wa Nje ili afanye uhakiki. *Epukeni kuzalisha hoja.*

- Wekeni mikakati na mipango madhubuti kuhusiana na mapungufu yote yaliyojitokeza ili kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo yote ya ukaguzi unafanikiwa. Mikakati hiyo inatakiwa iwe na uhalisia kiutekelezaji; itekelezwe kwa muda uliopangwa na iweke bayana namna ya utekelezaji.

- Halmashauri itenge Bajeti ya kutosha ili kuweza kuwapeleka Wahasibu na Wakaguzi kwenye Mafunzo ya mara kwa mara yanayoendeshwa na wataalamu wa Ufungaji wa Hesabu ili kuweza kupata miongozo mipya na marekebisho yake (IPSAS).

- Halmashauri itoe kipaumbele katika maandalizi ya Hesabu za Mwisho kwa kuhakikisha waandaaji wanawekewa mazingira mazuri wakati wa zoezi hilo na kuwaondolea mwingiliano kati ya jukumu hilo na majukumu yao mengine ya kila siku.

- Menejimenti ya Halmashauri iimarishe udhibiti wa ndani na mara kwa mara ifanye tathmini ya vihatarishi vya udanganyifu ili kubaini na kuzuia udanganyifu kabla haujatokea.

- Menejimenti ya Halmashauri ihakikishe Taarifa ya Fedha inaandaliwa kwa usahihi na kuzingatia miongozo na viwango vinavyoelekezwa.

- Afisa Masuuli ahakikishe unakuwepo uhusiano mzuri/ushirikiano kati ya Menejimenti ya Halmashauri na Wakaguzi wa Nje na wahakikishe nyaraka zote zinazohitajika zinapatikana kwa wakati.

- Fanyeni uhakiki wa ubora wa kitabu cha hesabu za mwisho kabla ya kuwasilisha kitabu husika kwa Mkaguzi.

MASUALA YA KUZINGATIA

Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri,

Masuala yafuatayo yazingatiwe:

i. Wah. Madiwani wapewe taarifa kila robo mwaka kuhusu Ukaguzi wa Miradi na hali ya Utekelezaji wa Miradi husika (ukilenga uwepo wa *Value for Money*) kwa kipindi hicho. Taarifa hizo zitokane na Ukaguzi uliofanywa na Kamati ya Fedha na Uongozi, Mkaguzi wa Ndani na ule uliofanywa na Kamati ya Ukaguzi wa Miradi ambayo huongozwa na Afisa Mipango.

ii. Taarifa za Ukaguzi wa Miradi zijadiliwe na pale itakapobainika kuwepo kwa dosari, hatua za haraka za kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa wahusika. Nakala za taarifa hizo ziwasilishwe Ofisini kwangu.

iii. Zingatieni Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utekelezaji wa Majukumu yenu. Katika eneo hili mnaongozwa na Kanuni za Maadili ya Madiwani na Kanuni za Maadili kwa Watumishi wa Umma. Ni utovu wa Maadili

na ni uvunjaji wa Sheria kwa Wah. Madiwani na Watumishi wa Umma kutumia nafasi na Madaraka yao kujipatia Mikataba na Zabuni mbalimbali ni makosa pia kwa Viongozi na Watendaji kutumia vibaya fedha na mali nyingine za Serikali.

iv. Simamieni ubora na viwango katika Miradi inayotekelezwa kwenye Kata zenu. Nawashauri muwakemee Watendaji wasiozingatia ubora katika usimamizi wa Miradi inayotekelezwa na pale inapobidi Mamlaka zishauriwe kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma.

v. Zingatieni ratiba za vikao katika ngazi zote na hakikisheni Mikutano Mikuu ya Vijiji, Kamati za Maendeleo za Kata (WDCs) na Mabaraza ya Kata inafanyika. Iwapo Mikutano hiyo itafanyika kwa kuzingatia ratiba zake (na pale inapobidi kwa dharura) changamoto mbalimbali zinazowakabili Wananchi katika maeneo yenu zitapatiwa ufumbuzi.

vi. Simamieni na hakikisheni fedha kwa ajili ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Walemavu zinatengwa na kutolewa kwa walengwa. Fedha hizi ni asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri (yasiyo ya masharti).

vii. Fanyeni tathmini ya kina ya uwezo wa vyanzo vyenu vya mapato na wekeni mikakati inayotekelezeka ya kuimarisha na kuboresha usimamizi wa mapato ili kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani

(katika mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri yenu ilikusanya mapato pungufu kwa asilimia 3 ya malengo ya mwaka). Kutokana na hali hiyo, Halmashauri yenu ilikuwa na uwezo wa kujitegemea wa **asilimia 7** tu (mlikuwa tegemezi kwa Serikali Kuu kwa **asilimia 93**). *Hakikisheni mnatumia vyema Mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya Mapato ili muweze kupata fedha za kutosha kuboresha huduma za jamii na kuchangia shughuli za maendeleo.*

viii. Afisa Masuuli ahakikishe Wakuu wa Idara na Vitengo wote wanahusika katika utoaji wa taarifa muhimu kwa ajili ya kuandaa taarifa ya fedha. Afisa Masuuli anapaswa kuhakikisha ubora na usahihi wa taarifa zinazowasilishwa kwa ukaguzi.

ix. Afisa Masuuli aimarishe na kufuatilia kwa karibu utendaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (kwa kutoa fedha za kutosha, mafunzo na vifaa/vitendea kazi) na kuimarisha Ufanisi wa Ukaguzi wa Ndani kama sehemu ya mfumo wa udhibiti wa ndani ya Halmashauri.

x. Afisa Masuuli aimarishe Kamati ya Ukaguzi (kwa kutoa fedha za kutosha, mafunzo na vitendea kazi) na ahakikishe inatimiza majukumu yake kikamilifu katika uangalizi wa mifumo ya utoaji taarifa za kifedha, taratibu za kusimamia athari zinazotokana na shughuli za kifedha, udhibiti juu ya utekelezaji wa sheria, maadili, kanuni na taratibu. Kamati ya Ukaguzi inapaswa kufanya Vikao kila robo mwaka kwa kuzingatia

matakwa ya Sheria na Kanuni ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

xi. Halmashauri iboreshe mfumo wa utunzaji nyaraka, hii ikiwa ni pamoja na kutenga chumba maalum kwa ajili ya kutunzia nyaraka za fedha na manunuzi. Aidha, ateuliwe mtumishi mmoja makini atakayehusika na utunzaji wa nyaraka mbalimbali za fedha zikiwemo hati za malipo.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri,

Kwa kuhitimisha, natoa msisitizo kwamba;

- Halmashauri iimarishe usimamizi wa vyanzo vya mapato na ufuatiliaji wa makusanyo ili mfikie malengo ya mwaka ya makusanyo. *Kuweni wabunifu na ibueni vyanzo vipya vya mapato*.

- Zibeni mianya yote ya upotevu wa mapato na chukueni hatua za kisheria na kiutawala kwa wote watakaobainika kuhujumu ukusanyaji wa mapato. *Katika hili, hamna sababu ya kumvumilia Yeyote.*

- Imarisheni Idara ya Fedha, Kitengo cha Sheria, Kitengo cha TEHAMA, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na Kitengo cha Manunuzi kwa kuwasiliana na Mamlaka ili waweze kuletwa Watumishi wa kutosha na wenye sifa stahiki za kielimu na kimaadili.

- Boresheni utoaji huduma na tatueni kero za Wananchi kwa wakati. *Hapa ninawaomba Wah. Madiwani mjiwekee utaratibu wa kutenga siku moja kwa wiki kusikiliza kero na Malalamiko ya Wananchi katika Maeneo yenu na kuyatafutia ufumbuzi.*

- Endeleeni kutenga fedha za mapato ya ndani na kuzipeleka kuchangia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa kuzingatia kiwango kilichowekwa.

- Imarisheni uwezo wa Wakuu wenu wa Idara na Vitengo kwa kuwawekea utaratibu wa kupata Mafunzo kazini kuhusu masuala ya Menejimenti.

Akhsanteni kwa Kunisikiliza.

==========